



Unapokula samaki mtamu jua hatari anazokabiliana nazo mvuvi

Samaki wa aina hii aliyekaangwa ni mtamu kumla lakini upatikanaji wake unahitaji ujuzi mzuri wa matumizi ya vyombo vya kuvua majini. Picha zote na Nashon Kennedy, Mwanza

Na Nashon Kennedy

VIONGOZI wa kitaifa, kijamii, kisiasa, wataalamu, watu walio kwenye vikao vya maamuzi na wananchi mara nyingi wamekuwa wakikaa mezani wakila chakula kwa kitoweo cha samaki mwenye ladha tamu kwa furaha.

Ili kitoweo cha samaki kikamilike na kuandaliwa mezani, yupo mtu ambaye hufanikisha mchakato mzima wa kupatikana kwa kitoweo hicho cha samaki na huyo si mwingine bali mvuvi mdogo.

Mvuvi huyu licha ya juhudi ambazo huzifanya akiwa majini kumtega samaki, anakumbana na changamoto nyingi ikiwamo dhoruba kali, imani za uchawi, hatari za wanyama wakali na kubwa zaidi ikiwa ni changamoto ya vifo vinavyotokana na kuzama majini.

HALI HALISI

Tafiti za awali zimebainisha kuwepo kwa viwango vya juu vya kufa maji miongoni mwa wavuvi katika ziwa, lakini ni mambo machache tu yanayofahamika kuhusu sababu kuu za vifo hivyo.

Tafiti za awali zimebainisha kuwepo kwa viwango vya juu vya kufa maji miongoni mwa wavuvi katika ziwa, lakini ni mambo machache tu yanayofahamika kuhusu sababu kuu za vifo hivyo kwenye familia na jamii za wavuvi.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2016-2018 kwa jamii za wavuvi katika Ziwa Victoria na Taasisi ya MITU kwa kushirikiana na Shirika la Royal National Life boat (RNLI) la Uingereza, ulibaini kuwa wavuvi 1,500 kati ya wavuvi 100,000 hupoteza maisha kwa kuzama.

Katika utafiti huo,

matukio ya wavuvi kuzama maji yaliyotokea ziwani yalikuwa 217 kati ya watu 100,000 na 86 ya waliofariki walitambuliwa, 70 ikiwa ni sawa na asilimia 81 walikuwa wavuvi, kati ya hao wakiwa na umri wa miaka 18-40 walikuwa ni wanaume na tisa walikuwa ni watoto wenyume umri chini ya miaka 10.

Kati ya wavuvi waliozama ziwani ni wavuvi wawili tu kati ya 86 waliovaa jaketi okozi (life jacket) wakati walipopata changamoto za kuzama maji na kutokana na athari za kijamii na kiuchumi za vifo hivyo, zilisababisha kupotea kwa mapato na kuvunjika kwa familia.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) wa kuzuia watu kuzama duniani wa mwaka, watu 236,000 hufariki kwa kuzama majini kila mwaka na vifo vyote vya kuzama maji vililwalenga zaidi watu walio chini ya umri wa miaka 30.

Kwa mujibu wa utafiti huo, wanaume walikuwa na uwezekano wa kuzama mara mbili zaidi ya wanawake na ulibaini kuzama maji kwa watu ni moja kati ya sababu 10 zinazongoza kwa vifo duniani.

Akiwasilisha matokeo yaliyotokana na utafiti shirikishi jamii uliofanywa na Shirika lisilo la kiserikali la Emedo kwa ufadhili wa RNLI kuanzia Mei hadi Desemba 2021, uliokuwa na lengo la kupata taarifa zinazosababisha wavuvi kuzama na kufa, athari za vifo vinavyotokana na kuzama kwa jamii za wavuvi (kijamii na kiuchumi) kwa familia na mitazamo ya jamii, Mratibu wa Mradi, Anthur Mgema anasema utafiti huo uliofanyika mwaka jana na kujumuisha makundi mbalimbali ulibaini sababu

za wavuvi kuzama majini na kufa maji.

Mgema anayataja makundi yaliyoshirikishwa kwenye utafiti huo kuwa ni wavuvi, wachakataji (wanawake na wanaume), mama lishe, wasomba ngese, wamiliki wa mitumbwi, mafundi watengeneza mitumbwi na viongozi wa mialo (BMU).

Makundi mengine ni viongozi wa serikali ngazi za kata na wilaya, maofisa maendeleo na uvuvi, wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya usalama majini na wachuuzi wa samaki.

"Kwenye utafiti huo tulizingatia sababu za kijiografia, kina cha maji katika ziwa, aina ya uvuvi unaofanyika na ukaribu na maji," anasema Mgema.

MATOKEO YA UTAFITI

Mgema anasema utafiti huo ulibaini sababu hatari zinazosababisha wavuvi kuzama maji ambazo zimegawanyika katika makundi tofauti kwa mtu mmoja mmoja, kwa mamlaka, utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni.

Anasema utafiti huo ulibaini kuwepo kwa matumizi hafifu ya vifaa vya usalama kwenye maji mfano jaketi okozi na vifaa dira, vyombo duni vya uvuvi ikiwemo mitumbwi isiyokidhi ubora, upepo na dhoruba kali, kulegalega kwa utendaji wa BMU na kutopewa kipaumbele kwa taarifa za hali ya hewa.

Mengine ni wavuvi kuesha mitumbwi bila kuwa na kiashiria chochote kama taa au tochi na kulala ziwani, kuwepo kwa mbinu duni za kutafuta na kuokoa linapotokea tukio la kuzama maji, ujuzi hafifu wa kuongoza vyombo vya majini hasa mitumbwi, imani za kijadi, ubebaji mizigo kupita kwa kiasi kwa mi-

tumbwi, baadhi ya wavuvi kutojua mbinu za kuogelea na kujiokoa na matumizi makubwa ya pombe wakati wa kuvua.

"Tulibaini pia kuwepo kwa matumizi ya mbao zenye ubora hafifu katika kutengeneza mitumbwi," anasema Mgema.

Anasema baada ya utafiti huo, wamebaini kuna athari nyingi zitokanazo na vifo vinavyotokana na kuzama zikiwemo familia za wavuvi kusambaratika na kukosa huduma muhimu kama elimu, matibabu na chakula, ndoto za watoto katika familia kukosa mwendelezo, vipato vya familia kuterereka na kuongezeka kwa wategemezi katika familia.

MITAZAMO YA JAMII

Mgema anasema utafiti huo umebaini jamii ina mitazamo tofauti juu ya jamii za wavuvi kuzama maji ikiwemo kuona ni kitendo cha kawaida, wengine kuhushisha na imani za kijadi, mtu akijua kuogelea havezi kufa maji, uzembe binafsi na kutojali na kuna mitazamo kuwa ziwa hu-meza watu.

Anayataja makundi yaliyobainishwa kwenye utafiti kuwa kwenye hatari kubwa ya kuzama maji kuwa ni wavuvi wenyewe, wanawake wachakataji samaki na watoto wanaofanya shughuli za uvuvi maeneo ya visiwani.

"Tuliwasilisha matokeo ya utafiti huo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuonesha hali ilivyo ya wa-

vuvi katika ziwa," anasema Mgema.

BAADA YA UTAFITI

Anasema baada ya utafiti huo, Emedo kwa kushirikiana na Shirika la Lifeboat wameanzisha mradi wa miaka mitatu (2022-25) wa udhibiti wa kuzama maji kwa jamii za wavuvi ujulikanao kama "Lake Victoria Drowning Prevention Project", ukiwa na lengo la kutoa elimu juu ya matukio ya kuzama maji kwa jamii za wavuvi katika Ziwa Victoria.

Anasema mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika mkoa ya Mwanza wilayani Ukerewe katika vijiji vya Irondo na Musozi na Wilaya ya Nyamagana katika Mtaa wa Sweya, mkoani Mara katika Wilaya ya Musoma katika vijiji vya Busekela na Kome na mkoani Kagera mradi huo unatekelezwa katika Wilaya ya Muleba katika visiwa vya Goziba na Mulumo.

Anasema mradi huo unaofadhiliwa na RNLI, shirika lenye uzoefu wa miaka 200 ya shughuli za uokozi na elimu ya usalama kwenye maji, una lengo kwamba ifikapo mwaka 2025 wadau wa sekta ya uvuvi wahakikishe wanachukua hatua madhubuti za kudhibiti vifo vitokanavyo na kuzama maji kwa jamii za wavuvi zinazoishi kuzunguka Ziwa Victoria.

Anasema muhimu ni kuwa shughuli za mradi huo zimezingatia mahitaji ya jamii, mazingira husika, mkakati madhubuti na vipaumbele vya mfadhili na

uwezo wa kibajeti kwenye utekelezaji wa mradi.

SHUGHULI ZA MRADI

Mgema anasema katika awamu ya kwanza mradi utajikita zaidi katika kutatua changamoto zinazosababisha kuzama kwa jamii za wavuvi na kuangalia namna gani shughuli za wavuvi zitafanikiwa.

"Mradi huu unatarajia kufanya uchechemuzi wa kisera na kisheria kwa masuala yaliyoibuliwa kwenye utafiti na yatakyoi-buliwa na jamii wakati wa utekelezaji wa mradi na utatoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi na wataalamu wa uvuvi.

MAONI YA WADAU

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Emedo, Editrudith Lukanga anasema anawataka jamii kuunganisha juhudi za pamoja ili kudhibiti matukio ya kuzama maji kwa jamii ya wavuvi hapa nchini kwa ajili ya ustawi wa maisha yao.

"Wavuvi watambue maisha yao ni dhamana yao, wasivae jaketi okozi wakati wanapowaona maofisa uvuvi, hali hiyo haiwakomoi maofisa uvuvi bali wanajikomoa wenyewe," anasema na kuongeza kuwa Emedo itashirikiana na BMU katika kuhakikisha usalama kwa wavuvi.

Mwenyekiti wa BMU, Sweya Petro analipongeza Shirika la Emedo kwa kazi nzuri ya utafiti waliofanya ambao utasaidia jamii na taifa katika kuwasaidia wavuvi kuwa salama majini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la Emedo, Editrudith Lukanga (wa pili kulia) alipoutambulisha mradi mpya wa miaka mitatu wa kuzua vifo vya wavuvi vinavyotokana na kuzama maji katika Ziwa Victoria kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah (wa pili kushoto), hivi karibuni ofisini kwake jijini Dodoma. Kulia ni Mratibu wa mradi huo, Anthur Mgema.